

# HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA

BARUA ZOTE ZITUMWE KWA MKURUGENZI MTENDAJI (W) S.L.P 88 NGUDU

SIMU: 028-2983121,  
Nukushi: 028-2983119  
Barua Pepe: dhro@kwimbadc.go.tz  
ded@kwimbadc.go.tz  
Tovuti: www.kwimbadc.go.tz

S.L.P 88,  
NGUDU / KWIMBA

Tarehe: 03/05/2021

Wananchi wote,  
Wilaya ya Kwimba,  
S.L.P. 88,  
**NGUDU/KWIMBA.**

## **YAH: TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA**

Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Kwimba anawatangazia nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira.

Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi ya Ajira wanateuliwa kwa Mujibu Kanuni 128 na 130 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003, ambapo kila Mjumbe atashika wadhifa kwa muda wa miaka (5) isipokuwa kama kuna sababu za kusitisha, na atakayeteuliwa badala yake atashika nafasi hiyo kwa kipindi kilichobaki.

### **Sifa zinazotakiwa:**

Mwenyekiti atakayechaguliwa na Halmashauri lazima atoke miongoni mwa wakazi wa kawaida ndani ya eneo miliki la Mamlaka ya Serikali za Mitaa atakayekuwa na uelewa wa mambo ya Utumishi, Utawala na Sheria.

### **Majukumu ya Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira:**

- (1) Kuongoza Vikao vya Bodi ya Ajira kwa Mujibu wa taratibu ya Vikao hivyo.
- (2) Kusaini Muhtasari wa Kikao cha Bodi ya Ajira

## **Mshahara**

Mwenyeketi wa Bodi ya Ajira atalipwa stahiki za Kikao kwa mujibu wa Waraka wa Utumishi wa Serikali Na.2 wa Mwaka 2010 wenye Kumb.Na.C/AC.17/45/01/125 wa tarehe 11/02/2010 ukisomwa kwa pamoja na Waraka wa Watumishi wa Serikali Na.4 wa mwaka 2014 wenye Kumb.Na.CAC.17/45/01/G/103 wa tarehe 02/12/2014

Masharti ya jumla ya Mwombaji

- i) Awe Raia wa Tanzania ambaye ni mkazi au mzaliwa wa Wilaya ya Kwimba
- ii) Awe na Elimu ya Utawala, Sheria au Utumishi
- iii) Waombaji waambatishe vivuli vya vyeti vyao vya shule, Taaluma, kuzaliwa/kitambulisho cha Uraia(NIDA) na Wasifu (Curriculum Vitae).
- iv) Kila Mwombaji aambatishe picha ndogo (passport size) zilizopigwa hivi karibuni
- v) Kila Mwombaji aandike kwa usahihi Anuani yake na namba ya simu inayopatikana muda wote.

Maombi yote yatumwe kwa:

**Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya.  
S.L.P. 88,  
KWIMBA.**

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 09/05/2021 saa 9:30 Alasiri.

Imetolewa na;



Stamili A. Ndaró.

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA KWIMBA.**

*MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA*

Nakala:

Watendaji wa Kata,  
Halmashauri ya Wilaya,  
**KWIMBA.** - Weka kwenye mbao za matangazo